The Connection

Kuwaleta wanafunzi pamoja na waadhiri tangu 1998

Montague & Associates 2007
CEO: Mr. Jeffrey Montague
-Chuo Kikuu-

Rais-Anthony Giratore
Makamo wa Rais-Kristine Bompadre
Gazetti - Mwenyekiti: Rachel Frankwich
Wasaidizi: Irina Burakovsky, Morgan Finkelstein, Zachary James, Misuzu Mori, Jared Price, Angel Torres
Makadirio- Mwenyekiti:Eunice Muya
Msaididizi: Eric Gillman
Mikutano
Mwenyekiti: Marcus Lambert
Wasaidizi: Laurie Harrelson, Ashley Roucroft, Ira Young
Kuchangisha fedha- Mwenyekiti: Jessica Carolina
Wasaidizi: Travis Lentz, Robert Licata, Billy Plichta, Isaac Satten, Katelyn Wild, Reiri Yamaski
Idara ya wafanyikazi - Mwenyekiti: Sara Nolan
Wasaidizi: Jason Colon, Christina Deckhut, Scott Grissell
Idara ya Uuzaji- Mwenyekiti: Christopher Fields
Wasaidizi: Dana Dommermuth, Kadie Grisola, Tahoe Kim, William Koskinen
Mradi - Mwenyekiti: Kacee Lawver
Wasaidizi: Kristine Bompadre, Anthony Delgott, Ryan Ganley,Maiko Iwasaki, Chou Lee, Lauren Quick
Udhamini- Mwenyekiti: Kristin Youse
Wasaidizi: Marisa Judge, Mark Kniley, Chuck Young
Wenye Kujitolea/CPR - Mwenyekiti: Mark Vasquez
Wasaidizi: Lisa Katzmar Curtis Kaucher, Momoko Yoshida

-Chuo Kikuu Mjini-

Rais-Mackenzie Tolliver
Makamu wa Rais-Bethany Whitstone
Newsletter- Mwenyekiti: Jessica Stern
Wasaidizi: Oana Bugariu, Mike Burns, Danielle Goffredo, AsukaHara, Timothy Lilley
Makadirio - Mwenyekiti: Jenna Heasley
Msaidizi: Thomas McNicholas
Mikutano
Mwenyekiti: Jason Jiau
Wasaidizi: Kim Berardi, Leanda Rinehart
Kuchangisha fedha - Mwenyekiti: Catherine Morris
Wasaidizi: Chris Baker, Louise Castellano, Jared Corra, Kelly Golderer, Alison Williams
Idara ya wafanyikazi- Mwenyekiti: Kym Langham
Wasaidizi: Mike McMahon, Viviane Rabelo
Idara ya Uuzaji - Mwenyekiti: Eliza Stasi
Wasaidizi: Colin Dempsey, Becca Fest, Jessica Hummel, Kerry Houck
Mradi- Mwenyekiti: Michael Goldstein
Wasaidizi: J'hannel Becoat, Becky Cohen, Toshiaki Enoki, Tristen Gabel, Allison Perlstein
Udhamini - Mwenyekiti: Nicole Ouimet
Wasaidizi: Alexis Hahalis, Jeremy Mortoroff , Jessica Smeriglio
Wenye Kujitolea/CPR/Wadadisi Nyota- Mwenyekiti: Antonio Sciulli
Wasaidizi: Diana Ciglar, Joy Okoro

Ujumbe Kutoka Kwa Marais

Hamujambo,

Tunawakaribisha wanafunzi wapya na wanaorejea kwenye jarida la chuo kikuu cha Temple University School of Tourism and Hospitality Management. Toleo la jarida hili linaweka mtazamo wake kimataifa na ulimwengu mzima. Uhusiano wa maisha yetu ya kila siku umeshikamana kwa njia ya magari tunayoendesha, bidhaa tunazozinunua, vyakula tunavyokula pamoja na teknolojia. Mengi ya mambo haya yana uwezo wa kutuunganisha ulimwenguni kote. Kama wanafunzi wa chuo cha utalii na makaribisho maridhawa, tuna fursa ya kufikia ulimwengu kupitia taaluma yetu, na nafasi tunazopewa kupata mazoezi nje.

Madarasa ya wanafunzi wanaoleke kuhitimu katika masomo yao wana furaha kuanzisha muhula wao na kuanza safari yenye changa moto na kufanyika wataalam wenye talanta. Tuko na idadi ya mambo yatakayofanyika tukijumuisha *siku ya utendaji kazi wao tarehe 7 Novemba 2007*, na siku ya kujulisha itakayokuwa tarehe 6 Desemba 2007. Matukio haya yote yanampa mwanafunzi fursa ya kukutana na kuunganishwa na wataalam wa viwanda kukiwa na matumaini ya kupata uzoefu wa siku za usoni katika ulingo wa spoti kuzalisha makaribisho maridhawa na utalii.

Mwaka wetu wa kifunzi umewadia na inaonekana kama mwisho wa safari na ndio mwanzo wa utendaji kazi yetu viwandani. Siku ya utendaji ya kazi waipendayo, ili wasije wakatamaushwa kazi hata siku moja katika maisha yao. Kwa kusema tunawapa changamoto wanafunzi wapya na wanaorejea wajihusishe na chuo cha utalii na makaribisho maridhawa, na wajumuishe kwenye maeneo ya viwanda a wachukue hatua ya kupanga siku zao za usoni

Kama marais wa warsha ya kufuzi tunatazamia kufanya muhula mkuu na waajabu.
Wenu,

Anthony Giratore
Rais Chuo kikuu

Mackenzie Tolliver
Chuo kikuu mjini

Ndani ya toleo hili…

Kuhamazishwa kitamaduni……2-3
Starehe……..4-5
Utalii/Usafiri……..5-8
Michezo ya Kimataifa……...8-11
Toleo la Utaaluma……11-14

School of Tourism and Hospitality Management
TEMPLE UNIVERSITY

Kuhamazishwa Kitamaduni

Uungana wa Kitamaduni

Na:Eliza Stasi

Biashara la kimataifa ni swala linalokuwa kwa haraka kwenye tamaduni za leo. Tunategemeana zaidi katika misingi ya kimataifa sasa kuliko awali. Unaposafiri kimataifa, iwe kwa swala la biashara au binafsi ni muhimu kuelewa tamaduni ya nchi unayozuru. Kwenye safari yangu Italia majira ya kiangazi, nilitazama kwa karibu utofauti wa kitamaduni kati ya wataalamu vijana katika maeneo ya utalii na tamaduni zingine ili kuhakikisha heshima yetu na kukubalika kwetu tunapokumana na watu wa mataifa mengine.

Tendo rahisi la kutikisa kichwa kuashiria ‘ndio’ au ‘la’ linaweza kuwa dhihirisho tosha la kuonyesha kutokuwa na heshima katika taifa la Wayunani. Kwenye tamaduni za Wayunani, wanelewa kwamba kutikisa kichwa kwelekeza juu kunaashiria ‘la’, na kupinda kichwa kushoto au kulia kunadhihirisha ‘ndio’ Tendo lingine katika nchi ya Marekani la kuinua kidole cha gumba kunaashiria ‘sawa’ pasipo kutamka neno, ila hali kwa Wayunani kunaashiria lugha chafu.

Nilipohudhuria kazi ya nje ya kujifunza ungwani nilijifunza kwamba kumsalimia mtu kwa mkono kunaonyesha kuwa wewe ni mtu mwenye msimamo na mwenye nguvu. Kumsalimu mtu kwa mkono ulio imarika kulitiliwa mkazo kila mara na msemaji wetu wakati unapokutana na kusalimiana na wataalam wa kibiashara. Hii huenda ikawa ndiyo hali ya mikutano ya kibiashara za kinyumbani, lakini ijapo katika biashara ya kimataifa, kila tamaduni wana njia yao ya kipekee ya kusalimiana. Unaposafiri Itali kwa ajili ya biashara, utakuta unapewa busu kwenye shavu moja badala ya kusalimiwa kwa mkono. Salamu ya mkono ulioimarika si ya kawaida ukiwa Hong Kong kama ilivyo Marekani. Karibu kila mkutano wa kibiashara unahitaji aina Fulani ya kugusana kama njia ya mawasiliano. Kwenye tukio nyingi, salamu hizi ziko kwenye hali ya kusalimiana kwa mkono. Hata hivyo, zinatofautiana nchini India. Wanaposalimiana Wahindi wenyewe hutumia ‘Namaste’. ‘Namaste’ hutukia wakati viganja vya mikono vimeletwa pamoja kimo cha kufua na kuinamishwa kwa kichwa kidogo.

Wamerikani huwa makini kujipa nafasi, mstari fulani ukivukwa kunatokea hali ya kutokuwa na amani ndani yao. Ufanyapo biashara Sweden, wanatilia maanani nafasi ya mtu binafsi. Wasweeden ni waangalifu kupeana nafasi mmoja kwa mwingine, ila hali Italia inaweza kuhesabiwa kuwa tendo la ujeuri na kutokuwa na heshima ukikosa kumkumbatia au kumsogelea mtu kwa karibu.

Kujifunza tamaduni zingine ni jambo la muhimu katika ulimwengu wa leo, na wala sio tu kwenye shughuli za kibiashara, bali pia kwa ajili ya maisha ya kila siku. Kufahamu zaidi juu ya watu wanajomuisha ulimwengu tunamoishi ni swala nyeti katika kwa kuelewa tamaduni zingine zinavyotumika. Kwa maelezo zaidi juu ya ya utamaduni na ungwana tafadhali tembelea tuviti ya www.adiplomat.com au hudhuria mankuli itakayofanyika tarehe 9, Oktoba 2007 ambayo imeandaliwa na chuo cha utalii na makaribisho maridhawa.

Pasi ya Ufanisi

Na: Kelly Golderer

Katika dira ya jumuia ya leo, uwezo wa kusafiri kwa uhuru kuvuka mipaka umekuwa na muhimu kuliko hapo awali. Kampuni mbali mbali zimeongeza kiwango cha biashara zinazofanyika ng’ambo na hivyo basi, kuleta haja ya kuwakilisha katika maeneo hayo. Kumiliki pasi ya kusafiria kunaonyesha waajiri umejitolea kuboresha biashara, unakumbatia nafasi ya kusafiri na kupanua ufahamu wa kampuni ulimwengu kote. Kwa kumiliki pasi, kunaashiria waajiri kwamba umejifungua kwa tamaduni mpya. Mbinu za kisasa zinadai wasimamizi wawe wazi kwa tamaduni ili kuboresha huduma za kisasa kwa watenda kazi tofauti tofauti.

Kwa sababu ya ucheleweshi unaotokana na shirika la uhamiaji la Marekani, ni muhimu kuomba pasi haraka iwezekanavyo. Kuomba pasi sasa kutakuondolea vizuizi vingi siku za usoni. Ikiwa utahitaji kusafiri kimataifa ghafla basi utakuwa umejiandaa. Kwa kujiandaa utakuwa umeonyesha umejipanga na una moyo- vitu viwili vya uthamani kwa viongozi wa leo.

Punde tu unapopokea pasi, ni muhimu zaidi kuhakikisha ya kwamba iko katika muda wa kutumika . Pasi huisha muda na nilijifunza jambo hili kwa njia ngumu wakati wa kiangazi niliposafiri kwenda Japan. Kwa kupanga safari yangu kuelekea ng'ambo nilichukulia maanani taratibu za kupokea stakabadhi ya kusafiria, kwa sababu tayari nilikuwa na pasi. Mipango yangu ya kusafiri ilikatizwa ghafula wakati mhudumiwa wa uwanja wa ndege wa Milwaukee aliponijulisha singeweza kuabiri ndege kwa sababu pasi yangu ilikuwa imeisha muda. Ikiwa ningechukua muda kuthibitisha stakabadhi zangu za kusafiria, ningeokoa kiwango kikubwa cha pesa na muda. Kutoka uwanja wa ndege wa Milwaukee, niliendesha hadi Chicago, nikaifanyia kazi pasi yangu na nikarejea siku iliyofuata nikaabiri ndege kuelekea Japan.

Nashiriki masaibu hayo yangu ili wengine wasirudie makosa kama haya yangu. Kumiliki pasi ni ya muhimu katika ulimwengu wa kisasa.

Fanya hima. Hakikisha siku zako za usoni, na omba pasi yako leo. Unaweza kuomba pasi ukiwa katika chuo chetu cha Temple University. Ofisi za huduma za kimataifa zinahudumu kama shirika la kupokea maombi ya pasi ya Wamarekani. Kuomba, lazima upange ratiba ya kuonana. Njoo siku ya kuonana pamoja na thibitisho la uraia wa Marekani, thibitisho ya kitambulisho , picha mbili ndogo za pasi nakiwango cha $67, kama ada pamoja na $30 na utendaji kazi. Unaweza leta na hundi au ulipe kupitia shirika a posta.

WANAFUNZI WA MWAKA WA KWANZA!
Angalieni Ann and Randy Hart Scholarship na upokee pasi bila malipo.
www.temple.edu/studyabroad/students/hartscholarship.htm

Fursa Ulimwenguni: Chuo Kikuu cha Temple ng'ambo

Na: Mike McMahon

Chuo Kikuu cha Temple kina fursa nyingi za masomo ng'ambo katika bara nne tofauti. Japan, Uhispania, Ufaransa, na Italia ni baadhi ya maeneo maridhawa unayoweza kwenda na kuendeleza masomo yako huku ukikutana na, na kufurahia tamaduni mpya. Jumanne 13 Novemba, Chuo cha Temle kitasheherekea nafasi hizi za ajabu kwenye tamasha ya pili ya kila mwaka kwenye kongamano lao. Chuo cha Temple kitazungumzia wanafunzi watenda kazi na waalimu, na ratiba kutoka ulimwenguni kote . Kupitia mazungumzo ya wadadisi, makaratasi ya picha, filamu na maonyesho ili kusisitiza vipengele vitatu vye endelevu: Utafiti wa wasomi, ubunifu wa wachoraji, na huduma ya jumuia.

Masomo ya kimataifa, utafiti wa kimataifa, na jumuiko la ulimwengu ndiyo yatakayokuwa mada yetu matatu yatakayolengwa wakati wanafunzi wahadhiri na watenda wataleta elimu aina mbali mbali na ratiba za kubuniwa zilizo na ushawishi mkubwa kimataifa. Wakati wa kutoa toleo lao, watazungumzia ongezeko ulimwengu, viunganishi vya kuleta maendeleo kupitia mifano ya kimataifa la tukio la fursa hizi. Kutokana na tukio hili ulimwenguni, Chuo cha Temple kimepokea idadi kubwa ya wanafunzi kutoka mataifa mengine kuja kuhudhuria chuo hiki chetu hapa Philadelphia. Kama moja ya vyuo vyenye wanafunzi wengi tena wa kutoka tabaka mbali mbali. Wengi wa wanafunzi wa Marekani wamesafiri kwa mataifa mengine ili kupanua ufahamu wao wa ulimwengu na kukumbana na elimu kwa mwanga mpya.

Kwa yeyote mwenye kupenda kusoma kuhusu matukio ya ng'ambo, au angependa kuonja tamaduni mpya, tamasha za pili kila mwaka za chuo cha Temple zitafanyika katika Howard Gitties Student Centre tarehe 13, Novemba, 2007. Kongamano litaanza asubuhi na kutamatishwa adhuhuri na

onyesho la wazi, litakalojumuisha miziki mbali mbali kutoka ulimwengu kote. Hii ni moja ya fursa ambazo Chuo cha Temple kitatoa kwa wanafunzi mbali mbali.

www.temple.edu/studyabroad/globaltemple/conference.html

Starehe

Utelezi wa barafu Afrika Mashariki

Na: Eunice Muya

Mjini Nairobi Kenya, hoteli ya Panari Sky Centre inaweza kujivunia kuwa mwanzilishi wa mchezo wa kuteleza kwenye barafu ya kuhifadhiwa kwa kutumia nguvu za jua, unaoweza kutumiwa na watelezi 200 na kina kipimo cha futi 15,000 mraba. Kifaa hiki chenye kutumia jua kimewezesha wakenya wengi wenye nia ya kuhisi furaha ya kuteleza wakiwa na madhumuni ya kubuni mambo katika eneo la utelezi. Kituo hiki cha Panari kina vyumba 136 vya kifahari. Kama mgeni, unapewa fursa ya kutumia kifaa hiki cha utelezi kwenye barafu na huduma zake. Idara ya Utalii Kenya imechangia pakubwa ushuru ambao umeshika sehemu muhimu katika uchumi wao. Kuwa na kifaa kama hiki kwenye Panari Sky Centre itasaidia kukuza utalii kwenye maeneo kama haya, kwa wenyeji na watalii wa kimataifa.

Kwa wengi, wazo la kuteleza kwenye barafu Afrika mashariki laonekana kama ni uwongo, na wengi wamekuwa na shauku kama kifaa hiki kitafanikiwa kwa muda mrefu. Kwa wakenya wengi, ada ya kutumia kifaa hiki kwa lisaa limoja ni, ambayo ni shilingi 800 ($12) kwa watu wazima na shilingi 500 ($7) kwa watoto ni kiwango ambacho ni adimu kwa wakenya wengi. Swali ambalo linalohitajika kuulizwa ni kama kifaa hiki kilinuiwa kutumika na wale wenye mapato makubwa au watalii. Hata hivyo, kwa kuwa kifaa hiki kinaendelea kufanya vyema, hakuna ishara kwamba watu hawataki kulipa kiwango hiki ambacho ni cha juu kwa lisaa limoja. Lakini kwa sasa ni hemko inaendelea kwenye utelezi kwenye barafu, imebakia kuwa vutia kubwa kwenye wakazi wa Nairobi. Paradiso Panari.*The Standard*<www.eastandard.net.>.

Wote Ndani

Na: Isaac Satten

Kwa mara ya kwanza, onyesho la kiulimwengu la karata imepanuka kutoka kwa vyumba vya karata Marekani na kwa kweli kufanyika mchezo wa ulimwengu. Kufatana na matukio yaliyo fanyika kwenye Hoteli ya Rio na Jumba la karata la Las Vegas mnamo Juni 1- Julai 16, moto uliovuka ng'ambo ya Atlantiki ili kuendeleza kwa mara ya kwanza (Bara Uropa) Onyesho la ulimwengu la karata.

Tofauti na wenzao wa Marekani, watu wa Bara Uropa, tafsiri yao ya onyesho la ulimwengu, ilikuwa na tukio tatu pekee, kuwa chache ukilinganisha na michezo 55 za juma 6 kwenye mkusanyiko uliofayika Nevada. Tukio mbili za kwanza zilikuwa karata mbili za sifa, mchezo wa H.O.R.S.E. na kipimo nyungu Omaha. Mashindano yote mawili yalitwaliwa na watu wa Bara Uropa, huku Thomas Biel akitwaa taji la H.O.R.S.E. na Dario Alioto akitwaa taji la Port Limit Omaha. Hata hivyo mchezo mkuu ulikuwa ni wa No-Limit Texas Hold Em. Ndivyo ilivyokuwa mchezo huu ulidhihirisha sarakasi ya ushindi wa aina ya kipekee.

Akifanyika mchezaji mdogo kutwaa taji la onyesho la ulimwengu kwenye mchezo wa karata, mwanadada Annette Obrestad wa Norway mwenye umri wa 18, alijitwalia zawadi ya kwanza ya dhahabu iliyozoa pauni 1,000,000 ($ 2,013,102) katika hali hiyo. Baada ya ushindi wake Obrestad alinukuliwa akisema "Sikutarajia kushinda. Hata maneno ya kusema sina. Sijui niseme nini." Kama mwanadada, Annette Obrestad aliweka rekodi mbili kwa kushinda

mchuano huo, baada ya kushinda pesa nyingi katika mchuano kama mwanadada, na pia kuwa ushindi wa juu kwa mwanadada katika onyesho la dunia la karata katika historia. Ushindi wa Obrestad kwenye onyesho la ulimwengu, Bara la Uropa limeleta changamoto kwa kukoma kunakoambatanishwa na mchezo huo wa karata. Kamwe mchezo huo wa karata sio wa wanaume tu, bali ni vita vya ujuzi vilivyoandaliwa kwa yeyote mwenye mawazo, na pesa kujitosa ulingoni na kujaribu kushinda. Kuongezea, Annette, ambaye kisheria hangeruhusiwa kucheza karata hadi mwaka wa 2010, alidhibitisha ya kwamba, sio vigongo tu wa mchezo huo wa karata wlio na mono wa kushinda. Hata hivyo, washindi wote watatu wa karata Bara Uropa walikuwa wachanga ukiwalinganisha na idadi ya waliokuwa uwanjani. Mchezo huu ambao hapo awali ulihifadhiwa kwa Wamarekani, sasa umekuwa ni mchezo wa ulimwengu mzima. Twakupongeza Annette, na twatazamia kukuona kwenye meza ya karata, miaka mitatu kutoka sasa.

Utalii na Usafiri

India iliyorembo?

Na: Kacee Lawver

India ni nchi ambayo imejulikana kwa maelfu ya miaka kuwa nchi ya vitoleo mbali mbali. Nchi ya kutunza tamaduni mbali mbali zenye rangi rangile katika kila sehemu ya maisha. Ulimwengu uliobakia una wazo kuhusu hii nchi yenye burudani zake, mahali ambapo maisha yanaangaziwa, pi urembo wa ndovu wanaorandaranda kwenye barabara. Hata hivyo, nilivyotambua mwezi wa Januari, India yenyewe haiko karibu na sifa iliyolimbukizwa kupitia picha zilizochorwa kwenye mawazo ya watu. Kama taifa linaloendelea, India iko katika kiwango cha kutumia mafikra ya watu wengine kupitia utalii na makaribisho maridhawa ambayo yamechochewa na ongezeko la kiuchumi kwa mwongo mmoja sasa.

Hata kwa hatua hizi, taifa hili limeathiriwa na kiwango cha chini cha kimaisha na hali ya kutogawa rasilmali kwa usawa.

Mwezi huu wa kwanza uliopita, nilishiriki katika ratiba ya hatima ya India kupitai shule ya Fox School of Business. Tulitumia muda wa siku kumi kusafiri hadi Mumbai na Goa ili kujionea hali ya Biashara tamaduni na matendo ya taifa linaloendelea na biashara zao. Mada ilikuwa ‘Strive for Globalization’ (Kujitahidi kuchangia maswala ya Ulimmwengu) Jukumu ya utalii na makaribisho maridhawa haingeweza kupuuzwa katika ukuwaji wa taifa hili. Japo utalii wa India umekuwa na umeendelea kukuwa, kuna vizuizi vingi ambavyo vinapaswa kuondolewa kabla India kuchangia katika utalii wa kiulimwengu. Njia moja ni kuboresha hoteli zao zifikie kiwango cha ulaya, kuboresha barabara zao, na kuwa muundo msingi wa taifa la India.

Serikali ya India inajishughulisha na jitihada za vipande vya taifa hili, kama vile Goa, ikuvutia watalii wa ulimwengu. Goa imeendelea kuliko maeneo mengine yote ya India, huku ikitoa huduma za mahoteli yenye viwango vya mataifa ya Magharibi. Fuo zao za bahari ni rembo na zinazotoa maeneo mwafaka kwa watalii kuondoa uchovu na kupata ladha halisi ya India pasipo kutatizwa na hali duni ya maisha na mamillioni ya wakazi wengine wa taifa hili la India. Vyakula vinavopatikana hapa Goa ni tofauti na vinavopatikana India. Watalii kutoka Marekani wakija hupewa vyakula vya kuwafaa kama vile nyama ya ng’ombe, ambayo huwa haizungumziwi, au kuitishwa kama chakula India. Huku ikionyesha kuwa ni taifa ya kitalii, Goa ilionekana kunyang’anywa sehemu yake tuliporejea katika mji wa Mumbai, mahali ambapo watu wanaishi katika nyumba zilizoundwa kwa kutumia mikebe, na ambazo hazina nguvu ya umeme, hata kuchimba mitaro kama sehemu ya barabara kukafanywa kwa kutumia sahani ndogo tu.

Ili kuongeza utalii kwenye taifa, wizara ya utalii ya India imebuni kampeni kabambe ya kutangaza India kwa ulimwengu mzima, ili kuwafanya wawe n a moyo wa kuja kutembelea taifa hili linaloendelea kuwa na kuwa na maonyesho mengi ya kitalii. Kampeni hii kabambe inachangia utalii katika njia mwafaka, huku ikitiilia maanani kubuni kazi ili pesa zipatikane kwenye mikono ya wanaofanya kazi ya kuendeleza utalii na makaribisho maridhawa nchini India. Kampeni hii kabambe inayojulikana kama 'Incredible India' (India iliyopita kiasi) inatazamia kuchangia utalii katika njia itakayofunza wengine sio tu kuhusu urembo wa nchi hii, bali pia kuhusu tamaduni zake. Lengo la kuzuru taifa kama India linahusu hisia tofauti, na sarakasi baina ya tamaduni ya mtu binafsi. Kama tukio , Wizara ya Utalii inauza India kama sehemu murwa ya kupumzika na kuondoa uchovu ambayo inatoa talii katika maneno yaliyoundwa na kuwaelekeza katika maeneo tofauti tofauti.Hata ingawa kulikuwa na nyakati zilizonifanya kutamani kurudi Marekani, matokeao haya yalinifumbua macho, nisitamani kubadilisha nilichoona na chochote. Nilijifunza mengi kuhusu India kwa kufanya mambo madogo kama kuwa macho nikisafiri kwenye basi masaa mengi na kutazama watu wakiendelea na shughuli zao za kila siku. Hali ya maisha ya watu ilinivunja moyo kila siku nilipowatazama. Hili ni taifa linaloongoza katika mambo ya kiteknolojia, ikiwa na majumba ya mtandao katika kila kichochoro, bali majumba duni ya watu pia yamepangana, na nilitazama vile walivotoka nje ya majumba yao yasiyokuwa na milango. Asubuhi, nilitazama mmoja akiwa amebeba besheni ya maji akielekea kuoga katika chumba kidogo cha majani alichounda; na ilikuwa ni wakati wa jua kuchomoza kwa kuwa hakuna nguvu za umeme ndani ya nyumba hizo. Pia nilitazama na kuona wanawake waliokuwa wakifua nguo kwenye mikusanyiko ya maji iliyotokana na mvua uliopita. Hili ni taifa linalohitaji pesa zinazopatikana kutokana na utalii, na serikali haijapuuza jambo hili. Kwa miongo kadhaa ijayo, kuna mipango kabambe ya kuimararisha hali ya mtazamo wa taifa hili kutoka nje, hususan kutilia mkazo kuwavutia watalii wenye madola, ambao wamekuwa adimu kuzuru taifa hili. India ilinivunja moyo lakini tamaa yangu ya kurudi na kuona hatua walizozichukua kimaendeleo bado zi pamoja nami. Ukitaka kuchukua hatua nje ya sanduku lako, basi nakushauri utembee India na uikumbatie tamaduni yao.

The McRiceburger: Uendelevu wa Kibiashara Taiwan

Na: Jason Jiau

Sote tujuavyo, inashangaza kuona jinsi uendelevu wa biashara ulimwenguni umekuwa, na jinsi inavyoendelea kushawishi maisha ya watu wengi kiuchumi na hata kitamaduni. Niligundua jambo hili zaidi hapo awali wakati nilipozuru nchi ya Taiwan kwa mapumziko miaka kadhaa iliyopita. Shirika la mkahawa la McDonald lina sifa tele za

kupanua biashara zao ulimwenguni kote na kuhudumia mabillioni ya watu kwa mapochopocho yao.

Siku ilikuwa ya joto na unyevunyevu, sawasawa na alasiri yoyote katika Kaohsiung, Taiwan (ambalo ndio jiji la pili kwa ukubwa katika Jamhuri ya Uchina) Uchungu wangu wa kuhisi njaa ulihitaji malisho kwa hivyo nilitoka kwenda kutafuta kitu cha kumega. Ni wapi pengine unaweza kupata chakula kwa bei nafuu, kwa upesi, na inayofahamika zaidi ya mkahawa wa Mickey D?

Mimi na kaka yangu tuliingia kataika mkahawa huo, na papo hapo tukatambua utofauti bayana na wenzetu wanataifa hilo. Jambo la kwanza tulilogundua ni usafi mahali hapo! Tukamsongea msajili ili tuagize na hapo tukapata waajiriwa

waliotuhudumia kama inavopaswa, kama wateja wenye kulipa (tendo ambalo mara nyingi limesahaulika na mashirika yaliyoanzwa Marekani) Baada ya kuagiza, mpokezi wa fedha alituwekea chakula chetu kwenye meza, na kukikagua mara mbili (kuhakikisha ikiwa kiko sawa), akafungasha mkoba wake kwa utaratibu, na kasha kwa upole alikabidhi kwetu. Nilipokuwa nikisubiri chakula, nikatambua ubao wenye kuandika bei ya vyakula ulikuwa na tofauti; ulikuwa umeratibisha na kujumuisha vyakula vya humo nchini, mkate wa mchele. Badala ya kuagiza mkate wa nyama ya kubingirishwa, mkate huu ulikuwa umeshikamanishwa katikati ya wali uliyopondwa wa keki.

Kutokana na hali hii, nilitambua kuwa huduma hubadilika kulingana na utofauti wa kitamaduni, na utalaam wa humo ni swala la muhimu kwa ufanisi wa uuzaji ulimwenuni kote. Ilikuwa ni hali ya kusisimua kulinganisha tabia kati ya Wana-Taiwan walioajiriwa. Jinsi waajiriwa hawa walivyoshughulikia kila ratiba kwa malengo, ilitofautiana na wale wanaopeleka kwa kasi, kwenye huduma za ndani na nje, kwenye matawi ya Marekani. Ubao uliopanuliwa kwetu ulionyesha tofauti ambazo tamaduni za humo zilizonazo juu ya mikahawa ya McDonald katika maeneo ya uuzaji.

Toleo hili halinuii kuaibisha jinsi huduma inavyotolewa na kusifu wenzetu wa Taiwan, bali ni kuonyesha utofauti katika tamaduni, kwa njia kubwa inayoweza kushawishi hata mashirika yenye viwango vya juu. Sasa kila mara uonapo, usikiapo, au pengine kufurahia mkate wa mchele, utakumbushwa uendelevu wa kibiashara ulimwenguni.

Mkahawa wa `s Baggers wafika kimo cha tatu.

Na: Ashley Roucroft

Mmiliki wa mkahawa Michael Mack, ndiye wa kwanza ulimwenguni kuunda huduma inayotolewa kwenye mkahawa pasipo wafanyikazi. Ikiwa na mkao wake mjini Nurenberg, Ujerumani, Mkahawa wa ‘s Baggers ndio wa kwanza kutoa huduma ya mashine kwa kuagizia. Badala ya kuhudumiwa na mhudumu, wageni sasa wanaweza kuagiza wenyewe kwa kubonyeza tarakilishi.

Tarakilishi hizi zimewekwa mbele ya viti wanavyokalia kwenye mkahawa huu na sehemu zake za juu za kunywea. Katika ulimwengu wetu ambao unaendelea kiteknologia, ‘s Baggers wanawakilisha mfumo mpya wa kuhudumia wateja. Michael Mack anasema ya kwamba, ubunifu huu mpya utabadilisha pakubwa viwanda vya vyakula. Mfumo huu unabuni njia mwafaka kwa wageni kuagiza kile wanachotaka na jinsi wanavyohitaji huku makosa yakiwa adimu. Mfumo huu sio tu kwamba umeendelea na kukadiria wakati unaohitajika, bali pia unasafirisha chakula kutoka orofa ya pili yenye jiko, ikitumia reli maalum yenye kuteleza hadi kwenye meza. Kutamatisha mgao huu wa kushangaza, chakula hutolewa kwa njia nyingi tofauti zenye rangi rangile za magari.

Lengo kuu la ‘s Baggers ni kuwa mbele ya kila mkahawa wa wastani, huku wakijitwalia jina la mkahawa wa ‘kiwango cha tatu’, hawajajitolea tu kushinda washindani wao ulimwenguni tu, bali wanataka kuwaacha na butwaa wageni wao. ‘s Baggers wanataka kuwafanya wageni wao watoshelezwe kwenye mkahawa wao zaidi ya mwingine wowote. Kwa ufahamu wa mkahawa huu, wanahisi ya kwamba mhuduma wa wastani huenda asitoe huduma ya 100% ambayo mgeni anapaswa kupokea. Kuinua kiwango cha ujuzi , ‘s Baggers wanahisi ya kwamba ni muhimu kupunguza idadi ya wafanyikazi. Kwa sababu ya kupunguza huku, mkahawa huu utaweza kuutana na haja na matarajio kwa kiwango kikubwa cha kutosheleza wageni wao.

‘s Baggers pia hutoa ladha mbali mbali kila juma vyenye vitoweo vinavoandaliwa kwa njia maridhawa. Mkahawa huu hususan hutoa vyakula vyenye ladha ya Kifaransa, huku vikiwa na mpindo wa kvyake.Wao hutoa bidhaa ya mboga, au vyakula visivyotia mwili nguvi nyingi. Huku zikiwa na mafuta chache, na mafuta kidogo, vitoweo vyote ni vyenye ladha tamu. Waweza kupata vyakula vya

kuvutia na vinywaji vilivyoandaliwa kwa njia spesheli vinavyotengenezwa kutokana na matunda ya machungwa au mvinyo, uliogemwa na mizabibu kwa bei nafuu.

Michael Mack anaamini ya kwamba njia hii mpya aliyoibuni, itaunda soko mpya ulimwenguni kwa wenye mikahawa. Mkahawa huu mmoja wa kipekee ambao unaweza kupokea wageni 100 kwa wakati mmoja, huwa nafasi zake zimetwaliwa kila usiku! Mkahawa huu mpya ambao unaendelea umekuwa toleo la kutetemesha. Ni katika ufanisi huu wa ‘s Baggers, ndipo Mack anahisi ya kwamba anaweza kusafiri ng’ambo na kupanua biashara hii yake. Pia kuna duru za kuaminika ya kwamba huenda akajitoa kwenye ulingo wa biashara ya vyakula vya haraka ulimwenguni. Kulingana na Mickael Mack, alisema hivi “Hapa ‘s Baggers, chakula kwa upesi hufanyika chakula kizuri. Uthamani haukosi na ujuzi hauna mwisho.”

Michezo ya Kimataifa

Uwanja wa michezo wakaidi sheria za ardhi

Na: Marisa Judge

Najua umewahi kuona moja; uwanja wa michezo ukiwa na muundo wa matofali na sanamu za waliobobea kwenye michezo zikiwa zimetapakaa kote. Zinasifiwa kwa jina ‘viwanja maridhawa vya michezo’. Ukienda kwa sehemu kubwa utapata viwanja vya waliovuma kale. Lakini, ukiwaza bustani ya citizens Bank, au uwanja wa Lincoln Financial ndio unaoongoza, basi hebu lisha macho yako kwa kutazama majenzi ya Estadio Chivas, iliyo na makao yake mjini Guadalajara, nchini Meksiko. Uwanja huu in nyumbani kwa timu ya kandanda ya Las Chivas. Uwanja huu wa Chivas (ukijumuisha sehemu ya kusakata kabumbu, sehemu ya mashariki, na maeneo yaliyotengwa) inaundwa ndani ya volkano. Mviringo mweupe wa muundo msingi ambao umeshikamana wenye mviringo wa volkano utatoa moshi wenye kuinuka wenye kufanana na mvuke uliorushwa na mlima huu, kulingana na wenye maono haya Jean Marie Massaud na Daniel Pouzet.

Mawazo ya kuvutia ya uendelevu kwenye studio ya Massout Pouzet kule Ufaransa, na kampuni itayojulikana ulimwengu mzima HOK, wameshikamana kwa pamoja ili kuzindua ujenzi huu ambao utakaidi sheria ya ardhi. Uwanja huu wa michezo unaundwa kwa madaraja. Kwanza, sehemu ya ndani ya volkano imechimbuliwa, na uundaji umepewa muundo msingi imara. Jambo lingine ndani ya volkano hii ni karakana ya uuegezaji magari. Njia ya wachezaji kuingia, wasimamizi wa uwanja na mashabiki, umepindwa ndani ya viambazi. Bakuli, mahali ambapo uwanja wa kabumbu utakuwa umetandazwa, na viti vya mashabiki wa kushangilia hapo Chivas, vimewekwa ndani ya volkano. Uwanja huu wa michezo wa Chivas, utabeba takriban 45,000 na umeundwa kufanya wawe na starehe, sehemu 315 za kibinafsi, na sehemu 222 kama nafasi za walemavu na wanaowasukumia gari zao. Uwanja wa Chivas utakuwa na sehemu ya kuegezea magari 8,000 ya mashabik. Vitengo maalum vya nje kwenye uwanja vinavutia kama sehemu ya ndani. Kutakuwa na zaidi ya maduka 100, na sehemu za kunywea, kando na mkahawa mkubwa kwenye Uwanja wa Chivas. Uwanja wa Chivas pia utakuwa na sehemu ya filamu, maduka y kuuza bidhaa mbali mbali kama vile nguo, na maduka ya urembo kama vile vinyozi na saloni. Zaidi ya runinga 850 za HD-TV zitawekwa kwenye vyumba, vyoo, na maeneo yote ya uwanja huu. Kwa kuongezea, ubao wa picha utafunika maeneo yote ya sanduku na kujipanua katika sehemu tatu ya uwanja, huku ikijirejesha kwenye dari na kuonyesha picha, ujumbe na kutoa matangazo kwa mashabiki.

Sehemu ya uwanja itahifadhiwa kwa kiwango cha chini cha fedha kuliko viwanja vya hapo awali ambavyo vimekuwa vikihitaji utunzaji wa mara kwa mara. Uwanja wa Chivas, utakuwa ukichezewa kwa hali iliyoundwa, nyuzi, changarawe ilioboreshwa kwa njia maalum, na uwanja wa raba, na matoleo ya viatu vilivyoundwa mara ya pili. Muundo wa uwanja huu umeundwa ili kupitiliza maji kutoka uwanja na kustahimili miale ya kiangazi, na kupinga bacteria.

Shamrashamra zinazozunguka mtazamo wa uundaji huu ndizo zinazoonekana katika mji wa Guadalahaja. Kwa mujibu wa Jean Marie Massoud na Daniel Pouzet, mipango kabambe imewekwa

kuunda orofa ya kuishi katika mji huu. Hata hivyo, Massoud na Pouzet wakitambua ya kwamba watu wa Mexico wana uhusiano maalum na ardhi wamepanga kuweka muundo huu sambamba na tamaduni za hapa. Basi gundua kifaa kusichofanana na kingine kile, Gundua Uwanja Chivas. Huu ndio mchanganyiko kamili wa ubunifu na dunia. Unaweza kuangalia tuvuti ya uwanja huu kwenye:

www.estadiochivas.com.

Michezo ya Kimataifa ya ndani kupitia Sahani

Na: Rachel Frankwich

Stefan Szymanski ni mwanauchumi ambaye ana taaluma ya kusomea uchumi na biashara ya michezo. Baada ya kupokea shada ya Phd kwenye chuo cha Birkbeck, alifanya kazi katika Chuo cha Biashara cha London. Kwa sasa, anafanya na Chuo cha Biashara cha Imperial, London. Szymanski amefanya kazi katika toleo mbali mbali na ameandika vitabu titatu. Toleo la hivi majuzi linajulikana kama “National Pass-time” la pili ni “How American play baseball” na la tatu “The rest of the World plays soccer” akiwa imeandikwa kwa usaidizi na Andrew Zimbalist, ikizungumzia juu ya historia ya michezo na jinsi tuliyofikia mahali tulipo leo.

Katika mahojiano na Szymanski, niliweza kujifunza kwa nini aliamua kujitoa kwenye ulingo wa uchumi wa michezo na nikapata mtazamo wa ndani, na maoni ya mapendeleo yake katika michezo ya kimataifa.

Ni nini kilichochangia wewe kutamani kutoka kwa njia ya tamaduni ya uchumi na kujishughulisha na biashara ya michezo?

Najiona kama mwenye tamaduni za kiuchumi, na mwenye ujuzi wa kiuchumi kwenye viwanda, kwa kukujibu kiwastani. Hii inamaanisha kuwa nasomea utangamano wa kibiashara na wanunuzi kwenye soko. Ilifanyika tu kwamba nilipata taaluma ya kusomea biashara na mbinu zake za kipekee, ligi ya michezo. Pia, nina uelevu wa kihistoria wenye mabadiliko ya kibiashara na shughuli yake.

Ukiwa na ujuzi Marekani ya kaskazini na michezo ya kimataifa, utafauti wao wa juu kwenye michezo ni upi?

Katika kiwango ya ligi, changamoto kubwa ni kupanda daraja na kushuka daraja, ambapo timu ambazo hazifanyi vyema zinashushwa kwenye daraja ya chini, na zile ambazo zinafanya vyema katika daraja ya chini, zinapandishwa katika daraja ya juu. Katika Bara Uropa, watu huwaza jambo hili kama la kawaida katika mtazamo wa mashindano haya ya michezo. Il hali Marekani, watu wengi hawaelewi jinsi mambo haya hutukia.

Utofauti kwenye mpangilio wa kimataifa (kwa mfano ligi kuu) kulinganisha na Marekani ya kaskazini kwenye viwango vya mashindano vya kimataifa na / au kiwango cha ufanisi wa biashara ya michezo imejuwaje?

Kupandishwa daraja au kuteremsha daraja inaunda kiwango kikubwa kwa mashindano ya kiuchumi baina ya timu zinazoshindana, na wala sio kama utimilifu wa kushindana kiuchumi kwenye vitabu, mahali ambapo ligi zilizofungwa, ni kama uchumi wa kipekee na kutegea sehemu moja. Hii inamaanisha ligi zenye nafasi ya kupandishwa na kuteremsha daraja mara chache hutengeza pesa, bali ligi zisizo teremsha au kupandisha daraja hutengeneza faida kubwa. La kufurahisha, hata hivyo, ni kwamba sehemu zote za mashindano zina ufanisi kwa kuleta mashindano ambayo mashabiki hufurahia.

Wamerekani kila mara huzungumzia swala la mishara, 'sawazisha kiwanja', je swala hili la mishahara litawahi kujumuishwa katika ligi kuu na ifanikiwe?

Kama kungali kupandishwa na kuteremshwa daraja, kufanikiwa ni vigumu. Kwa nini timu ichezeshe kikosi ambacho hakijashinda mahasimu wao ikiwa hii itamaanisha watakuwa kwenye hatari ya kuteremshwa daraja na kujiunga na ligi ya chini ambayo hatimaye italeta mapato ya chini?

Katika mazungumzo ya kazi yako umezungumzia NASCAR kama njia mwafaka na mpangilio bora wa kusimamia michezo. Na ni kwa nini NASCAR ndio njia madhubuti? Je unaamini NASCAR 'mfano bora' inaweza ikabadilishwa na mpangilio wa michezo iliyo sasa?

Naweza nikasema ni madhubuti, lakini nafikiria kutangamanisha uongozi wa ligi na mashindano baina ya timu mbali mbali, huhakikishia mwongozo kwenye mashindano. Wenye vilabu ni mara chache kuweza kukubaliana wanapotoa sera zao, wakati wanapokea uamuzi wa pamoja, na hivyo basi kutangamanisha usimamizi wa ligi kama jambo inaweza kuchangia kutoa uamuzi bora. Baada ya yote, hatutarajii wachezaji Wimbleodon au wanagofu katika U.S Open waamue sheria na masharti ya michezo.

Marekani tunapata mchezo kuwa ni sehemu kubwa ya kuburudisho, hivyo basi tunaamua kutumia kiwango kikubwa cha pesa ambazo tumepata kwa michezo. Je unadhani matumizi ya pesa kimataifa ni kidogo au kingi katika matukio ya michezo? Na ni kwa nini?

Katika ulimwengu wa uchumi, tunafafanua kifaa cha starehe kama moja ya mapato inayoweza kubadilika na ya kuitisha zaidi ya 1, yaani, 1% ya ongezeko ya mapato huelekeza kwa ongezeko ya 1% katika matumizi. Starehe ya michezo ni kifaa cha fahari. Matumizi yapo juu Marekani kwa sababu ya kiwango cha juu cha mapato na malipo. Hata hivyo, Bara Uropa na Japan hazijaachwa nyuma, na pia kuna uwezekano mkubwa katika Uchina na India.

Mchezo kama wa kriketi ambao huvutia watu wa mapato juu, je unaamini masaibu ambayo hupata michezo katika mataifa ni tofauti na yale ambayo yako hapa Marekani?

Usiamini misemo ya watu. Kriketi ndio mchezo wenye sifa nyingi nchini India miongoni mwa matajiri na masikini. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba mchezo wa kuvutia pesa huegemea na kuvutia mabwenyenye na watu wa wastani ili kuzalisha faida nyingi. Ninaamini hii ni kweli kwa India (ambayo inkisiwa kufika millioni 300) kama Marekani.

Michezo ya Olimpiki inapokaribia London, kuna gumzo juu ya matumizi zaidi ambayo inaendelea kuonekana na kwa gharama kuu ya michezo huku kukiwa na idadi kubwa ya watu katika maeneo ya London. Je Unaamini michezo hii itakuwa na mafaa au kuegemea au kudhuru hali ya kiuchumi, na ni kwa nini?

Sina shaka London itathamini michezo hii kwa njia ya ufanisi, lakini pauni billioni 9 (dolla billioni 18) ambayo inakisiwa kuwa makadirio ya pesa zitakazotumika, italeta ufanisi wa kufana na wa kudumu. Vifaa vyenyewe havitatumika sana na nyingi ya fedha zitapatikana kutoka mchezo ya kulipia, ambazo kwa njia zingine zitakuwa zimetumika katika majengo ya michezo, na majengo ya kitamaduni ya jumuia ya waliodhoofika Uingereza. Hivyo tutalipa gharama kubwa kwa majuma matatu ya vishasha na mihemko.

Kwa kuwa ongezeko la kigaidi limekuwa kimataifa, tunaona upungufu mkubwa wa watu wanaonuia kusafiri. Je unadhania hii haitaathiri michezo ya kimataifa?

Sina uhakika sana ikiwa ugaidi umeongezeka sana kimataifa. Shambulizi za kigaidi katika olimpiki ya

Munich zilikuwa 1972, hiyo ni miaka 35 iliyopita. Na wakati huo tukikuwa na PLO, Baader – Meinhof, ETA, na IRA wote wakilipua, wakiteka nyara, na kuua. Kuna ugaidi kidogo leo ukilinganisha na miaka ya 1970. Kwa hivyo, hatari kwa ndege moja, au msafara mmoja iko chini ukilingaisha na wakati ulipita. Hata hivyo, matukio yataendelea kutokea, na yakitokea yatakuwa ya kuathiri kwa muda mfupi, na wala sio zaidi ya hivyo kwa mtazamo wangu. Ikiwa umependezwa na swala hili, basi tafuta kitabu kipya cha Stefani Szymanski na toleo alilochapisha. Kwa wale wangependa, tembelea tuvuti ya:

www3.imperial.ac.uk/people/s.szymanski

Jumuisho ya Wataalam/Mashirika

Shirika linaloongozwa na wanafunzi lachangia mambo mbalimbali

Na: Joy Okoro

NATIONAL SOCIETY OF MINORITIES IN HOSPITALITY

Huku ikiwa imekamilisha miaka mitatu pekee, Chuo Kikuu cha Temple chenye kushugulikia utalii na makaribisho maridhawa (STHM) katika shirika la kimataifa la makabila madogo yenye makaribisho maridhawa (NSMH) kinajikakamua kushinda hadi kiwango cha juu katika sehemu hii – kama shirika mpya linaloongozwa na wanafunzi, wenye taaluma, ambao wanashirikiana ndani ya STHM, NSMH inafanya kazi kwa bidii kuinua viwango vya watu wa tabaka mbali mbali kama inavyodhihirika kwenye chuo cha Temple, na vile vyuo vya satellite. NSMH ilibuniwa mwaka wa 1989 katika Chuo Kikuu cha Cornell. Historia yake inaambatana na uanzilishi wa nafasi kwa Waafrika na Kimarekani kwenye maeneo ya kitalii na makaribisho mariwadha. Hivi karibuni shirika hili limebadilisha mtazamo wake kuelekea kuunga mkono ongezeko la shirika lao ulimwenguni, na pia kuliendeleza ili liwe la kimataifa na la watu wa tabaka mbali mbali. Tangu ibuniwe, NSMH imejibadilisha na kuwa shirika kuu lenye wataalamu wenye ujuzi wa wakaribisho maridhawa, huku ikiwa na wanachama 1000 marekani kote.

NSMH ni msisimko mkubwa wa kirasilmali katika idara ya makaribisho maridhawa. Kitaifa, NSMH inatoa mwelekeo wa viunganisho, kazi, na fursa za nafasi za kuweza kufanya kazi maeneo mengine. Kila mwaka, NSMH hufanya mkutano wa maeneo na wa kitaifa, mahali ambapo wanachama wanaweza kukutana kwa udhamini wa makampuni, waakilishi wa viwanda, mashirika ya makaribisho maridhawa, washauri, walezi na wanafunzi wa vyuo vya upili ambao wataka kuendeleza ujuzi wao katika viwanda vya makaribisho maridhawa mwaka huu maeneo ya kaskazini magharibi, kongamano lao litafanyika Hartford, Connecticut, Oktoba 26-28. Mkutano wa 19 wa kila mwaka wa NSMH, mada yake itakuwa “MISSION POSSIBLE” (MALENGO YOTE YAWEZEKANA)
Utafanyika Februari 21-24, 2008 katika Jumba la Mikutano la Western, Pittsburgh,PA.

NSMH inawakilisha wanafunzi ambao watoka maeneo mbali mbali, kabila mbali mbali na tamaduni tofauti tofauti. Shirika kama hili huwapa wanafunzi fursa ya kujieleza na kuonyesha talanta za uongozi na kufungua fursa kwa marafiki zao. Hapa katika chuo kikuu cha Temple, NSMH inafanya kazi ya kuendeleza kikundi maalum kisichoegemea upande wowote na kinachowakilisha na kuelewa watu wa tabaka na tamaduni mbali mbali. Kwa kushauriwa na mkurugenzi anayejulikana wa viwanda na uhusiano bora Gregory DeShields, wa STHM Temple, kitendo cha NSMH bado kinatafuta wanachama wa kujaza kamati kwenye kitengo hiki maalum. Fursa hii imetolewa kwa wote, ikijumuisha wanafunzi ambao walishafuzu. Hii huenda ikawa nafasi yako ya kuchaguliwa.

Huku watu wa tabaka mbali mbali wakileta ushindani mkubwa katika viwanda vya makaribisho maridhawa NSMH ina uwezo wa kuweka mwanachama mmoja awe juu ya wengine, motto yao ikiwa “Mwanafunzi wa leo ndiye kiongozi wa kesho” Hii inaelezea kinagaubaga umuhimu wa kujishughulisha. Wanafunzi wote wa chuo cha Temple STHM wanastahili kujihisi wamechochewa kujihusisha na shirika hili litakalowasaidia. Kwa wale waliojihusisha, imewapa changamoto ya kuwaelezea rafiki zao wa STHM.

STHM yamkaribisha Dakt. Yvette Reisinger kwenye Idara.

Na: Bethany Whitstone

Chuo cha utalii na makaribisho maridhawa kina fahari kumkaribisha Professa Daktari Yvette Reisinger kwa Idara ya Chuo cha Utalii na Makaribisho Maridhawa, na Idara ya Usimamizi. Kabla ya kujiunga na chuo cha Temple, Dak Reisinger, alihudumu kama mkurugenzi na Makamukatika Chuo cha Makaribisho Maridhawa na Usimamizi wa Kitalii katika Chuo cha Florida kabla ya kufanya kazi katika chuo cha FIU, Dak Reisinger aliishi Australia kwa miaka 20. Alifanya kazi katika chuo kikuu cha Griffith, Gold Coast, Chuo Kikuu cha Victoria, Chuo Kikuu cha Melbourne, na chuo kikuu cha Monash, Melburne. Akiwa chuo cha Monash, Dakt. Reisinger alishikilia nyadhuifa katika utalii na mpangilio katika makaribisho maridhawa na pia kama mkurugenzi mkuu wa vyeti maalum katika Idara ya Makaribisho Maridhawa na Usimamizi.

Dakt. Reisinger alipokea shahada yake ya udaktari katika utalii na uuzaji kutoka chuo kikuu cha Victoria, mjini Melbourne, Australia. Pia ameshikilia shahada mbili za ujuzi mwingi (Masters). Shahada ya kwanza ni katika sekta ya Kitalii na Maendeleo Australia, na shahada ya pili ni katika Uchumi na Sayansi ya Jamii huku akiwa na utaalam katika Utalii wa Kimataifa katika Mpangilio na Tarakimu, nchini Poland.

Dakt. Reisinger anachukuliwa kuwa mtaalam katika matangazo ya kitalii na utafiti. Mchango wake katika utalii ni katika utafiti uwanjani katika tamaduni mbali mbali kwenye tabia za watalii, matangazo ya kitalii, kwenye sehemu, na kutangaza maneno ya kimataifa kwa watalii na pia ana ujuzi wa tamaduni mbali mbali za Wachina, Waindonesia, Wajapani, Wakorea na Waaustralia.Utafiti wa Dakt. Reisinger umewezesha kubuni maeneo ya kutangaza utalii kwa sehemu yake na mikakati inayolenga kuendeleza utalii wa Bara Hindi.

Dakt. Reisinger amechapisha kitabu kinachojulikana kama “Cross-Cultural Behavior in Tourism: Concepts & Analysis” ambacho kinalenga umuhimu wa kuelewa tamaduni na jinsi zinavyohusiana na utalii. Kitabu chake kinatumika kimataifa kama rasilmali, na wanafunzi wanaofuzu, pamoja na watafiti, na kimetafsiriwa kwenye lugha ya Mandarini. Yeye pia kwa sasa anaandika kitabu kinachoitwa “International Tourism, Cultures and Behavior”, ambacho kinzungumzia kwa nini wataalam katika sekta ya kitalii sharti waelewe utofauti wa kitamaduni, na jinsi utofauti wake unachangia utalii wa kimataifa na kuchochea watu kuzuru maeneo hayo. Kitabu kitatolewa katikati ya mwaka 2008.

Dakt. Reisinger anafunza masomo mawili ya chini muhula huu, kwanza. Maeneo ya Kutangaza pamoja na Utalii wa Kimataifa. Mtazamo wa maeneo ya kutangaza mafunzo yake, ni juu ya mapokezi yake kimawazo na njia mwafaka ya kusogelea maeneo ya kutangazwa katika taifa na mazingira ya kumataifa. Mtazamo wa mafunzo ya mtalii wa kimataifa uko katika uwezo unaoshawishi utalii wa kimataifa na hutuma maeneo ya utamaduni inayopatikana ndani yake.

Dakt. Reisinger ana matumaini ya kuingiza ndani ya wanafunzi wake umuhimu wa kuambatana na umakinikaji wa utalii wa ulimwengu. Pia anaamini ni ya muhimu kwa shughuli ya siku za usoni katika eneo hili la utalii. Kama mwanafunzi wa mafungo

haya yote mawili anayoyatoa, naweza kusema Dakt. Reisinger, utafiti wake wa kina, na ujuzi katika ulingo huu wa kitalii, ukijumuisha na ufahamu wake wa hali ya juu ya maeneo yote ulimwenguni umefanya kuwa dhamani la ongezeko kwenye shirika la STHM.

Karibu Dakt. Reisinger, Tunafuraha kuwa nawe!

HIFADHI TAREHE!

STHM Muungano wa Wanafunzi- Mkutano Mkuu
Tarehe: Oktoba 10, 2007
Saa: 3:40 alasiri
Eneo: SAC Room 200 A

Maonjo ya ziara ya Taifa
Tarehe: Oktoba 16, 2007
Saa: 3:30 alasiri - 7:00 jioni
Eneo: Drexelbrook Catering Center

Kongamano la 8 la kila mwaka - Fox School of Business
Tarehe: Oktoba 18, 2007
Saa: 8:00 asubuhi – 11:30 adhuhuri
Eneo: The Great Court at Mitten Hall

Sherehe ya Mavazi rasmi
Tarehe: Oktoba 28, 2007
Saa: 6:00 jioni – 11:00 usiku
Eneo: St.Monica's Bowling Alley
Mavazi rasmi yanahitajika

Mkutano wa kila mwakawa STHM- Siku ya Mtendaji.
Tarehe: November 7, 2007
Saa: 9:00 asubuhi- 12:00 adhuhuri
Eneo: The Great Court at Mitten Hall

Hamasisho – "Kuzunguka ulimwengu kwa usiku mmoja"
Tarehe: December 6, 2007
Saa: 6:10 jioni – 11:30 jioni
Eneo: Top of the Tower